Mkristo ni Nani Kulingana na Kile Ambacho Biblia Inasema? (Who is a Christiana According to what the Bible Says?)

Na

John Kombo

Mkristo ni Nani Kulingana na Kile Ambacho Biblia Inasema? (Who is a Christiana According to what the Bible Says?)

Na

John Kombo

January 8, 2013

Mkristo Ni Nani Kulingan Na Kile Ambacho Biblia Inasema?

Ninasoma jarida liitwalo, “Maandhari Mazuri ya Dini Duniani”; ndani yake kulikuwa na kipengele chenye kichwa cha habari “Ukristo Unamvuto Zaidi Duniani”. Alafu nikaanza kufikiri katika roho yangu, wote wanadai kuwa ni Wakristo je wote ni Wakristo wa kweli, kulingana na neno la Mungu lililoandikwa katika Agano Jipya?

Kwa kuyachunguza maandiko, yafuatayo ndiyo inayomanisha kuwa Mkristo, au kuwa katika Kristo.

Kama ningeitwa kutoa fafanuzi fupi na rahisi ya Mkristo, ningesema, “mtu aliye ndani ya Kristo”. Tunaweza kufahamu jinsi ilivyo vyema kuwa Mkristo kwa kufikiria inachomanisha kuwa ndani ya Kristo kama inavyopingwa kuwa nje ya Kristo.

Inachomanisha kuwa nje ya Kristo

Waefeso 2 inatoa fafanuzi ya Waefeso walipozifia dhambi (ms. 12): Wakati ule walikuwa “*hawana Mungu*” (ms. 12); hawakuwa na Baba mbinguni. Kuwa na MUngu kama Baba yetu wa mbinguni ni nyongeza (2 Kor. 6:17-18).

Walikuwa hawana Kristo (ms. 12). Hawakuwa na kuhani mkuu, hakuna Mungu wa Kumuomba, na hakuna Kristo kuomba kupitia; njia pekee ya kumfikia Mungu ni kupitia Kristo. (Yoh. 14:6). Mtu asiye na Kristo hawezi kufikia kiti cha enzi cha mbinguni.

- Hawakuwa na amani maana… ndio amani yetu (ms. 14)
- Hawakuwa na tumaini (ms. 12)
- Hawakujumuishwa katika taifa teule la Israeli (kiroho) (ms. 12)
- Walikufa katika ukosefu wao na dhambi (ms. 1)

Kuwa nje ya Kristo inamanisha kuwa upande wa mwovu; inamana kuwa katika utawala wake, “katika Kristo” na “katika uovu” moja ni elezo inayoelezea uwezekano wa uhusiano wa kiroho. Hakuna sehemu ya kati. Mtu ama yuko katika Kristo au kwa mwovu. Hapa tunaongelea watu wanaohesabika. Watu wanaoweza kupambanua katika ya mema na mabaya, mtu aliye na uwezo wa kuchagua.

Inacho manisha kuwa katika Kristo

Wale walio katika Kristo wana Mungu kwa sababu wamepatanishwa kwake katika mwili wa Kristo (kanisa la Bwana) (Efe. 2:16). Wakristo wana Kristo kama Kuhaniwa Mkuu. Sala ni baraka za kiroho katika

Kristo ikijumlishwa na ukombozi (Efe. 1:7), kuwa kiumbe kipya (2 Kor. 5:17), kupatanishwa (Efe. 2:16), na uzima wa milele (1 Yoh. 5:11).

Jinsi mtu anavyoingia katika Kristo

Mtu anapofundishwa kile inachomanisha kuwa nje ya Kristo, anapaswa kuuliza haraka, “Nifanye nini ili niwe ndani ya Kristo?” majibu ya swali hilo yanapatikana katika vifungu vya maandiko.

- “*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?*” (Rum. 6:3).
- “*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo Yesu mmemvaa Kristo.*” (Gal. 3:27).

Vifungu hivi vinaeleza kwamba tunabatizwa, “*katika Kristo*.”

Je ungependa kuwa Mkristo na kufurahia baraka zote ambazo hupatikana katika Kristo? Baada ya kusoma jarida hili, chukua hatua mhimu na ufanye maamzi ya kuwa “*ndani ya Kristo*” na kuwa Mkristo mwaminifu.

Mungu awabariki.

John Kombo Nandwa,

Kanisa la Kristo Baruti,

Nakuru, Kenya